BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 11 Septemba, 2026**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

183. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Moja ya miongoni mwa wajibu wa Mwakilishi ni kukusanya maoni kwa wananchi katika jimbo lake, ili kujua changamoto zinazowakabili na kuzisema.

Je, Jeshi la Polisi limepata wapi mamlaka ya kumzuia Mwakilishi kukutana na wananchi wake kwa lengo la kukusanya maoni.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

250. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kuna maeneo bado yanaendelea kumeguka kwa maji ya bahari kama vile Kilindini katika Shehia ya Micheweni. Hata hivyo, kuna Shirika lisilokuwa la Kiserikali limejitokeza kudhibiti hali hii.

Kwa kiwango kipi Serikali inalifahamu Shirika hilo.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

289. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kumekuwa na malalamiko kuhusu kauli zinazotolewa na baadhi ya viongozi au maafisa wa umma ambazo zinaweza kutafsiriwa kuwa vitisho, udhalilishaji au matumizi ya mamlaka yasiyozingatia haki na utu wa wananchi.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kushughulikia kauli au matendo ya viongozi na maafisa wa umma yanayoweza kuashiria vitisho, udhalilishaji au matumizi mabaya ya mamlaka.

(b) Je, ni hatua gani za uchunguzi na uwajibikaji zinazochukuliwa pale malalamiko ya aina hiyo yanapowasilishwa.

(c) Je, Serikali inawahakikishia vipi wananchi kwamba haki, usalama na utu wao, vitalindwa bila kujali wadhifa wa mtu anayelalamikiwa.

**<u>Wizara ya Kazi na Uwekezaji:</u>**

24. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kumekuwepo na kadhia ya wageni kadhaa wanaoishi na kufanyakazi katika ukanda wa utalii Mkoa wa Kusini Unguja hususani maeneo ya Paje, Jambiani, Bwejuu, Michamvi na Kizimkazi. Baadhi ya wageni hao wanadaiwa kumiliki hata makaazi ya kudumu.

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka husika dhidi ya wageni wa aina hiyo.

(b) Je, kwa kipindi cha mwaka unaomalizika, ni idadi gani ya wageni waliobainika kwa Zanzibar nzima, ambao wanaishi na kufanyakazi kinyume na sheria.

(c) Je, ni mikakati gani inawekwa ili kudhibiti matukio kama hayo ya wageni kuingia wanavyopenda na kuishi na kufanyakazi kinyume na sheria.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

18. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

    Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imekuwa ikifanya *intergration* baina ya mfumo wa VFMS na mifumo ya wafanyabiashara na wawekezaji, kwa lengo la kupata taarifa sahihi za mauzo, ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji kodi na *compliance*.

    (a) Je, ZRA imeshafanya *intergration* ya mfumo wa VFMS na mifumo ya hoteli kwa asilimia ngapi hadi sasa.

    (b) Je, hatua gani ZRA inachukua kwa biashara zilizoonesha vikwazo vya makusudi katika kufanya *integration* na mfumo wa VFMS.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

6. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

    Kwa muda wa takribani miaka 20, wadau wa Habari visiwani Zanzibar, wamekuwa wakililia kupatikana kwa Sheria Mpya ya Habari, ambayo itajenga misingi bora ya kuwalinda katika kutekeleza majukumu yao, pamoja na kuimarika kwa kazi na maslahi yao kwenye vyombo mbalimbali wanavovitumikia.

    (a) Ni sababu zipi zinazoikwamisha Serikali kuleta Mswada wa Sheria hiyo katika Baraza hili, kwa ajili ya kutunga sheria mpya.

    (b) Je, Serikali imefanya tathmini na kujiridhisha ni athari zipi zinazopatikana kwa kukosekana sheria hiyo katika utendaji kazi wa Waandishi, ulinzi na usamala wao.

    (c) Ni ipi ahadi ya Serikali kuhusiana na kuletwa kwa Sheria hiyo katika kipindi cha maisha ya Baraza hili la Kumi na Moja.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

168. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu, Jimbo la Ziwani limekumbwa na changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama hususani katika Kijiji cha Kwale, Niapi na Kichuuani (Shehia ya Kwale) na Shehia ya Ndagoni.

Je, lini Serikali itaitatua changamoto hiyo ili wananchi wa maeneo hayo waweze kuondokana na kadhia hii.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

220. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulifanya Zao la Karafuu kuwa ni zao la Taifa, wakati sasa umefika wa kutegemea zao jengine la Taifa letu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha zao jengine, ili kuwa na mazao mawili au matatu ya kitaifa.

**Wizara ya Afya:**

118. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Miongoni mwa matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ni Serikali kuwapatia wananchi wake matibabu bure. Hata hivyo, azma hii imekuwa haipatikani kama ilivyotarajiwa kwani bado wananchi wamekuwa wakitozwa fedha kwa ajili ya kununua dawa katika Vituo vya Afya vya Serikali.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea Vituo vya Afya vya Serikali kuendelea kuwatoza fedha za matibabu wananchi wa Zanzibar licha ya kuwa wanapatiwa huduma hizo kupitia Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) wenye kauli mbiu "Afya Bora kwa Wote".

(b) Ni utaratibu gani unaotumika katika kuvipatia dawa Vituo vya Afya vya Serikali.

(c) Kwa kuwa kauli mbiu ya Serikali ni kuwapatia matibabu bora na bure wananchi wake. Ni sababu zipi zinazopelekea Serikali kushindwa kutoa bure zile huduma ambazo hazipatikani kupitia Mfuko huo.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

206. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi;

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuja na mpango mzuri wa kisasa wa kufunga kamera njiani, ili kudhibiti ajali za barabarani na kuleta nidhamu ya matumizi ya barabara. Hata hivyo, wakati madereva wa vyombo binafsi wanaelekea kutii sheria za udhibiti bila ya shuruti, kumekuwa na tatizo kwa baadhi ya madereva wa vyombo vya Serikali kutotii sheria kwa kwenda mwendo wa kasi, kuegesha gari wanapotaka, kupita kwenye "zebra" bila kujali, kuvuka taa za usalama wapendavyo na kufanya viteno vyengine visivyokubalika.

(a) Je, Serikali imefanya uchunguzi wowote na kubaini uwepo wa tatizo hilo ambalo linalalamikiwa sana na watumiaji wengine wa barabara.

(b) Je, kuna sheria au maelekezo kwa madereva wa gari za Serikali kuwa wao hawaguswi na sheria za usalama barabarani.

(c) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kwa madereva hao wanaokiuka sheria za barabarani, ukizingatia kuwa, baadhi ya madereva hao ni wa viongozi kama vile Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na wakati mwengine hata baadhi ya Mawaziri na Naibu Waziri.

**Zanzibar,**
**11 Septemba, 2026.**

**(Ramadhan Khamis Juma)**
**KAIMU KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**